# KUWA MFUASI WA MTU



James Kalekwa

# KUWA MFUASI WA MTU.

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

Utangulizi.............................................................3

SURA YA KWANZA:  Kwanini uwe mfuasi wa mtu? . 5

SURA YA PILI:  Ngazi tatu za Kufuata watu................12

SURA YA TATU: Ufuasi ni nini?................................16

SURA YA NNE: Namna ya Kufuata............................. 17

SURA TA TANO: Thawabu ya Kufuata Mtu................22

SURA YA SITA: Ufuasi katika Utekelezaji.................. 30

Kuhusu Mwandishi:..................................................... 31

Kuhusu New Vine Church:........................................... 31

Mawasiliano na Mwandishi:......................................... 32

# Utangulizi

Moja ya siri ambazo ukizitambua, itakupa uwepesi na kasi isiyomithilika katika maisha ya kiroho, huduma na maisha kwa ujumla wake ni UFUASI. Na moja ya vita ambao adui amewapiga watu wengi ili kuwatenga na ukuu na hatima zao njema ni kufifisha au kuondoa kabisa uzito wa ufuasi ndani yao.

Watu wengi wako radhi na tayari sana kufuata… ila ni kumfuata Mungu! Lakini neno la Kristo, mahala pengi sana linazungumza kuhusu kuwafuata watu. Na huo ndiyo ujumbe mkuu kwenye kitabu hiki.

*"ili msiwe wavivu, bali mkawe* ***wafuasi wa hao wazirithio*** *ahadi kwa Imani na uvumilivu."* Waebrania 6:12

"Hao wazirithio ahadi" si malaika, si Roho Mtakatifu wala si Kristo Yesu… hao ni wanadamu kabisa! Kwa msingi huo, kila mtu anapaswa kuwa mfuasi wa "hao", yaani watu.

Umewahi kufikiri ya kwamba kwenye jeshi la uinzi na usalama kwenye nchi yeyote, huwa kuna mwanajeshi ambaye yeye huwajibika kwa amiri jeshi mkuu tu? Kwa wengine, hawajibiki? Hayumkiniki hata kidogo. Kila mwanajeshi anawajibika kwa kiongozi wake wa karibu "immediate leader". Hii ni kweli inayotokea kwenye msingi wa neno la Mungu. Unawajibika kumfuata mtu kabla hujawajibika kwa amiri jehsi mkuu.

Nimekuombea kwa Mungu wa mianga yote ya kuwa moyo wako utakuwa udongo mzuri utakaopokea mbegu ya neno la Mungu; hautaishia kusoma tu bali utachukua hatua za utekelezaji, kutendea kazi neno la Kristo. Hautaishia hapo bali utawasambazi wengine kitabu hiki.

Ninamwamini BWANA kuna jeshi la wafuasi wanaomaanisha, linainuka.

Hii nizawadi yangu kwako. Ni zawadi mahususi katika siku yangu ya kuzaliwa, 20 Juni, 2022.

Pastor James & Frida Kalekwa
New Vine Church – Dodoma

# SURA YA KWANZA:

# Kwanini uwe mfuasi wa mtu?

1. **Watu ni mawakili (custodians) wa neema mbalimbali**

*"Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu."* **1 Petro 4:10**

Jambo limewahi kunishangaza ni siku nilipoelewa andiko hili. Kwa lugha ya kiingereza neno mawakili ni "custodians" ambalo hutumika kwa namna nyingi ambazo ni pamoja na kumaanisha mwanasheria au msimamizi (hususani wa mirathi au mali za watoto wadogo). Kwenye andiko lililonukuliwa hapo juu, neno mawakili limetumika kumaanisha msimamizi wa mirathi/mali.

Sasa, lengo la msimamizi ni kushikilia mali mpaka pale wahusika/warithi watakapokuwa tayari kupokea sehemu ya mali yao.

Ndivyo ilivyo kwenye swala la neema. Huu ni uwezesho wa kiungu kutenda kwenye maeneo mbalimbali a kimaisha. Neno linaelekeza ya kuwa ,

neema haziko mbingu bali zimo duniani… na zimo kwenye maisha na utendaji wa watu!

Kama unazitaka neema unajua nini unatakiwa kufanya? Kuwafuata watu waliozibeba neema husika.

Hata ukimfuata Mungu, hatimaye, atakuelekeza kuwafuata watu kwa sababu neema amekwisha kuziachilia ndani ya watu. Hakuna namna utawakwepa watu na ukazipata neema!

Ni katika misingi hii huwa nina ujasiri wa kusema kufuata ni udhihirisho wa roho ya unyenyekevu ndani ya mtu. Watu wenye kiburi hawawezi kufuata. Kimsingi watu wadhaifu sana ndani yao, hawawezi kufuata!

## 2. Watu ni mwendelezo wa kivizazi wa mtiririko wa aina fulani ya maisha ya kiungu

*"Nikiikumbuka imani uliyonayo isiyo na unafiki, ambayo ilikaa kwanza katika bibi yako Loisi, na katika mama yako Eunike, name nasadiki wewe nawe unayo."* **2 Timotheo 1:5**

Kuna mtindo fulani wa maisha ya kifamilia na malezi kuhusiana na imani yanaonekana yakitirirka kwenye ukoo huu. Kiwango cha Imani isiyo na unafiki inaonekana ikihama kutoka kwa bibi Loisi, kwenda kwa mama Eunike kisha kumwagika kwa kijana Timotheo.

Ninachotaka uone ni huo mwendelezo/mtiririko kutoka kwa bibi mpaka kwa mjukuu. Jambo hili si la bahati mbaya hata kidogo. Mambo yoyote ya kiungu kwenye maisha huwa hayatokei tu kama bahati mbaya.

Ukiwafuata watu wa namna hii kama familia ya akina-Timotheo, utagundua tu ya kwamba unapaswa kwenda ueleko huo linapokuja swala la familia na imani.

Unakumbuka kisa cha Petro kumkana Yesu alipokuwa kwenye behewa ya kuhani mkuu? (Mathayo 26:69-75/Marko 14:66-72/Luka 22:56-62/Yohana 18:15-18, 25-27)

Waliomuona walimuhusianisha na Yesu Mnazareti; wengine na Yesu Mgalilaya… kwa kifupi Petro hata angejificha vipi angetambulikana bado ya kwamba huyu ni mfuasi wa Yesu Kristo. Ninachotaka uone ni kwamba Petro alifanana na Yesu mpaka kuongea kwake. *"...wewe ni mmoja wao, kwa maana usemi wako ni kama wao."* Mathayo 26:73b (Neno: Biblia Takatifu). Tunafahamu ya kwamba hatujawahi kusoma maandiko ambapo Yesu aliwafundisha wanafunzi namna ya kutamka maneno, kutunga sentensi, kuweka mianguko ya sauti kama Yeye. Hata hivyo, kwa kumfuata tu kila kitu kilimfanania Yeye.

Ukifuata kwelikweli, huhutaji kujitahidi kuwa. Utafanana na yule unayemfuata. Utageukia uelekeo wa yule unayemfuata! Hata wakati unamkana unayemfuata, utamkana kwa sauti kama yake!

### 3. Watu ni mwendelezo wa fundisho

*"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."* **2 Timotheo 2:2**

Fundisho (doctrine) na mafundisho (teachings) huwa yamekabidhiwa mikononi mwa watu.Ukitaka mafundisho kuhusu wokovu, maisha ndai ya Kristo, uinjilisti, imani, uponyaji, ndoa na familia, ustawi na maendeleo ya kimaisha, siku za mwisho, makanisa ya nyumbani, ufuasi, na mengineyo mengi… basi usijaribu kwenda mbinguni kuyatafuta. Kuna watu wapo duniani na wameaminiwa kuwa mawakili (custodians) wa mafundisho hayo. Hao ndiyo kama vituo vya mafunzo hapa duniani. Utakuwa na hekima sana ukiwafuata hao ili upate fundisho na/au mafundisho.

Angalia mnyororo wa kimafundisho ambao mtume Paulo anauweka; kwanza ni mambo ambayo Timotheo amesikia kwa Paulo. Asijaribu kuwa mgunduzi wa mambo yaliyogunduliwa tayari. Hayo anapaswa kuyahamishia kwa wengine. Ndiyo

kusema, Paulo ni kituo cha mafundisho. Kwa sababu ya ufuasi mwema wa Timotheo, akaaminiwa naye kuwa kituo cha mafundisho. Si kwamba hakukuwa na watu wengine waliosikia mafundisho ya Paulo, walikuwepo wengi sana. Mtume Paulo anawarejelea wengine kama "mashahidi". Walikuwa wengi kwenye madarasa ya mafundisho ya Paulo, lakini aliyetokeza kama kituo cha mafundisho ni mmjoa – Timotheo! Mungu akupe neema ya kutokeza kama kituo cha mafundisho katika jina la Yesu Kristo! Akaagizwa kuwakabidhi – siyo kuwafundisha… ni kukabidhi! Halafu hao waaminifu, yaani, vituo vingine vya mafundisho ndiyo waende kufundisha watu wengine.

Kama humfuati mtu yeyote, utakosa fundisho na hutakuwa na mafundisho. Kiburi kitayazika maisha yako. Nimekuombea kwa BWANA ya kwamba kiburi hakitakuwa fungu lako katika jina la Yesu Kristo!

## 4. Watu ni mwendelezo wa kazi na utume wa kiungu duniani

*"Musa mtumishi wangu amekufa; haya basi, ondoka, vuka mto huu wa Yordani; wewe na watu hawa wote, mkaende hata nchi niwapayo wana wa Israeli. 5. Hapatakuwa mtu yeyote atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako; kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa*

*pamoja na wewe; sitakupungukia wala sitakuacha.”* **Yoshua 1:2, 5**

*“Na Yehu mwana wa Nimshi mtie mafuta awe mfalme wa Israeli; na Elisha mwana wa Shafati wa Abel-Mehola mtie mafuta* ***awe nabii mahali pako****.”* **1 Wafalme 19:16**

Nimejifunza ya kwamba mitume (watu) huondoka duniani lakini utume (missions) huwa haziondoki mpaka zitakapotimilizwa. Unaona kwenye utume (mission) wa kuwatoa wana wa Israeli kutoka Misri kwenda nchi ya ahadi? Huko njiani, kiongozi mkuu aitwaye Musa aliondoka duniani, alikufa! Lakini utume alioubeba haukufa. Yoshua alipaswa kubeba kazi na kuendelea nayo mbele.

Si lazima kiongozi afe. Lakini kiongozi mmoja hawezi kuwa sehemu nyingi duniani kwa wakati mmoja – yeye siyo Mungu. Hivyo basi, kwa kumfuata mtu aliyebeba mission fulani, hata kama hautaki sana lakini tambua kuwa itafika wakati utaaminiwa kuwa mwendelezo (extension) wa utume huo kwenye eneo fulani la kijiografia – bara, nchi, mkoa, wilaya, kata, kijiji/mtaa.

Hebu tusogee mbele na ufunuo huu, ni kwamba Musa alikufa lakini Yoshua alipokea utume. Utajitendea haki sana kama utamuheshimu na kumfuata Yoshua, kwa sababu yeye ni mwendelezo wa utume! Kuna

utume upo unatenda kazi duniani saa hii na inawezekana umeasisiwa na kiongozi ambaye yuko mbali sana nawe kivizazi – ni wa kizazi cha kale; au yuko mbali nawe kijiografia. Usihangaike kumfikia yeye, wafuate watu ambao wanamfuata yeye. Wao ni mwendelezo wa utume alioubeba.

# SURA YA PILI:

## Ngazi tatu za Kufuata watu

1. Baba wa kiroho

*"Kwa kuwa ijapokuwa mna waalimu kumi elfu katika Kristo,* ***walakini hamna baba wengi****. Maana mimi ndimi niliyewazaa katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili."* 1 Wakorintho 4:15

Maandiko yanatuonyesha ya kwamba baba ni mmoja; ni yule aliyekuzaa kwa injili katika Kristo na anayahudumia maisha yako ya siku kwa siku katika ukuaji na ustawi wako.

Ngazi hii ya ufuasi inahusisha uwajibikaji wa moja kwa moja usio na kificho. Hapa ndipo unapopokelea fundisho (doctrine) na mafundisho (teachings) yanayoamua uelekeo wako. Hapa ndipo utatiwa moyo, utapendwa kwa karibu, utasaidiwa kuwa mtu bora zaidi ya hatua iliyopita. Huyu hukuamini na kukutengenezea majukwaa ili kudhihirisha kivitendo yale aliyokulea kwayo.

Usisahau hapa ndipo utapata maonyo na kukemewa kwa ukali kuliko ngazi yoyote ile. Hapa ndipo ambapo huwa panauma. Huyu ni mtu anayekumudu pamoja na ukubwa wako ulionao.

Watoto wengi sana huwatamani baba wa wengine kwa sababu tu hawajawasogelea kwa ukaribu. Kwa sababu

baba hafurahishi na pale ulipo, bali kule anakotaka uwe au uende. Basi, baba hukutoa kwenye utulivu na kukupeleka mahali kugumu zaidi kwa ajili ya ukuaji na ustawi wako. Utagundua, baba siyo rafiki yako; anaweza kuwa na mahusiano ya kirafiki *"friendly"* lakini usiwahi kujidanganya ya kwamba baba yako ni rafiki yako… baba ni baba!

2. Waalimu

*"Kwa kuwa ijapokuwa mna waalimu kumi elfu katika Kristo, walakini hamna baba wengi. Maana mimi ndimi niliyewazaa katika Kristo Yesu kwa njia ya Injili."* 1 Wakorintho 4:15

Hii ni zawadi ya watu ambao Mungu amewatoa kwenye mwili wa Kristo kuwa ni walekezaji. Kwa mujibu wa andiko hilo, kundi hili wanaweza kufika hata kumi elfu kiidadi, hakuna shida. Hawa kazi yao kubwa huwa ni kukuongezea na kujazia kwenye fundisho unalopata kwa baba yako.

Huwa ninapenda sana sentensi za mwanzoni asemazo mchungaji Matt Chandler wa The Village Church (TVC) anapokukaribisha kutazama video zake za mafundisho, *"...ninapendekeza ya kwamba mafundisho haya ya mtandaoni si mbadala wa wewe kujumuika kwenye kanisa la mahala pamoja. Mahali ambapo utajulikana na utachungwa kwa ukaribu. Tunashauri uyatumie kama*

*virutubisho vya chakula (suppliments) na si kama mlo kamili…"*

Kuna ngazi mbalimbali pia za kuhusiana na aina hii ya watu unaowafuata. Kuna wale ambao unaweza ukasoma, ukasikiliza na kujifunza kwao kutokea mbali. Lakini kuna wale ambao utahusiana nao na kujifunza kwao kiuwajibikaji. Kuna kuwa na mawasiliano ya karibu ya ujifunzi na kuhojiwa maswali; kuna kuwa na safari na mwelekeo fulani wa kujifunza.

3. Vielelezo

*"Lakini kwa ajili hii nalipata rehema, ili katika mimi wa kwanza, Yesu Kristo audhihirishe uvumilivu wake wote; niwe kielelezo kwa wale wote watakaomwamini baadaye, wapate uzima wa milele."* **1 Timotheo 1:16**

*"Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao wamainio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi."* **1 Timotheo 4:12**

Hawa ni watu ambao unawatazama na kujifunza kutokea kwao mambo mbalimbali ya kimaisha. Wanaweza wakawa wanajua au hawajui kwamba unawatazama kwa kujifunza. Hata hivyo, wao wanajua ya kwamba huwa wanatazamwa na watu. Inawezekana hawajui ni nani hasa anayewatazama, lakini wanatazamwa.

Wakati unatazama na kujifunza kwa wengine kama vielelezo, usisahau ya kwamba nawe kuna watu hukutazama hivyo pia. Uwe kielelezo!

# SURA YA TATU:

## Ufuasi ni nini?

Ni kuiga *"Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia neno la Mungu; tena, kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni Imani yao"* Waebrania 13:7

- Ni kuwa mfano wa *"Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo."* 1 Wakorintho 11:1
- Kuwa na nia moja na yule unayemfuata *"Maana sina mtu mwingine mwenye nia moja name atakayeiangalia hali yenu kweli kweli."* Wafilipi 2:20

- Ni kuwa mwendelezo (extension) wa utume, fundisho, mfumo wa maisha au mtu mwingine *"Basi nawasihi mnifuate mimi. Kwa sababu hii nimemtuma Timotheo kwenu, aliye mwanangu mpendwa, mwaminifu katika Bwana, atakayewakumbusha njia zangu zilizo katika Kristo, kama vile nifundishavyo kila mahali katika kila kanisa."* 1 Wakorintho 4:16-17

# SURA YA NNE:

## Namna ya Kufuata

1. Kwa kuangalia miisho, matokeo na shuhuda

Kufuata siyo swala la kishabiki na mashangilio yasiyo na maana. Siyo kwenda bila kutumia akili. Kwanza, unapaswa kuchunguza miisho ya unayemfuata – amemalizaje kazi? Kwa wale ambao hawajamaliza kazi angalia matokeo na matunda yao.

Nimeweka utangulizi huo awali kabisa kwa sababu, baada ya hapo unapaswa kuinamisha kichwa chini na kufuata kwa bidii. Kwenye madarasa ya ufuasi, si hekima tena kuendelea kuinua kichwa wakati unapaswa kufuata. Hii itaashiria tabia na madhihirisho ya uasi. Hivyo, hakikisha unaelewa ulipo kifuasi.

*"Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia neno la Mungu; tena, kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni Imani yao"* Waebrania 13:7

2. Kwa bidii

Ufuasi unapaswa kufanyika kwenye hali ya bidi. Na hii ni kwa faida yako wewe unayefuata. Kwa kadiri unavyoongeza bidi ndivyo utakavyopata thawabu zinazoambatana na ufuasi.

*“ili msiwe wavivu, bali mkawe wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa Imani na uvumilivu.”* Waebrania 6:12

Wafuasi wasiotia bidi kwenye kufuata, huumbuliwa na matokeo. Unaweza kuwa chini ya baba mzuri wa kiroho, ama ukajitiisha chini ya mwalimu mzuri au ukafuata kilelezo kizuri. Ikiwa hutaweka bidi kwenye kufuata kwako, hutakuwa na matokeo ya maana. Nisemacho ni hiki, ufuasi siyo ushirikina – kwa maana ya kutaka kuya-*“manipulate”* maisha! Sehemu yako ya kutenda kwenye mlinganyo wa ufuasi ni bidi yako binafsi.

*“Ni jambo moja kuwa chini ya kocha mzuri, na ni jambo jingine tofauti kuwa mchezaji mzuri”* Askofu Goodluck Kyara

3. Kwa namna anavyomfuata Kristo,

Muundo ule ule anaoutumia unayemfuata, kufuata ndiyo huo unapaswa kumfuata kwa kuutumia. Maandiko yanasema:

*“Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo.”* 1 Wakorintho 11:1

Hapa twaweza kuona ya kwamba mtu unayemfuata akiacha kumfuata Kristo basi amepoteza uhalali wa wewe kumfuata. Kipimo ni Kristo!

Pia, unaweza kuona ya kwamba muundo ni wa ufuasi ni ule wa kiongozi wako.

4. Kwa imani

Imani ni takwa la lazima kwenye swala la ufuasi. Kufuata ni udhihirisho wa juu wa utendaji wa Imani ndani yako unayefuata. Ukiondoa tu imani, utagundua huwezi kufuata.

*"ili msiwe wavivu, bali mkawe wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa **imani** na uvumilivu."* Waebrania 6:12

Mara kadhaa watu huuliza, *"Vipi kama ninayemfuata akibadilika?"*; *"Vipi kama ninayemfuata akiwa si mkweli?"*; *"Vipi kama ninayemfuata akikengeuka?"; …* nami huwa ninawauliza, "Vipi kama hayo (kubadilika, kutokuwa mkweli, kutokengeuka…) hayatatokea?" na kama hayatatokea na ukawa hujafuata, utakuwa umepishana na zawadi yako ya maisha. Hapo ndipo matumizi ya Imani yanapaswa kuingia kazini! Tunafuata kwa kichwa na kwa moyo… kwa kichwa tunachunguza miisho, na kwa moyo tunafuata huku tumeinamisha kichwa chini.

5. Kwa Uvumilivu

Ufuasi unahitaji sana uwepo na uhalisia wa tunda la Roho ndani yako – tunda la uvumilivu. Na hapa wafuasi wengi sana wametengwa kiasi cha kujikwaa. Unapomfuata mtu fulani, usisahau unamfuata **mtu**! Na kwa kadiri unavyomsogelea na kumfuata kwa karibu ndivyo

ambavyo unaona kwa uhakika ya kwamba huyo unayemfuata ni **mtu**… hata hivyo, kitabu hiki kinazungumzia kuwa mfuasi wa mtu. Kwani kuna ubaya wa mtu kuwa mtu? Hebu tazama maandiko matakatifu yanasemaje.

*"ili msiwe wavivu, bali mkawe wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa imani na* ***uvumilivu.****"* Waebrania 6:12

Uvumilivu unahitajika sana pale linapokuja swala la kuhusiana na watu. Hii ndivyo ilivyo hata kwa namna unavyohusiana na unayemfuata. La sivyo utapishana mbali sana na thawabu za ufuasi.

Mtu yeyote ambaye unamfuata ana pande mbili – upande wa uwakili wa neema mbalimbali; upande mwingine ni wa ubinadamu wake.

Hebu nikuonyeshe maandiko kadhaa hapa ili uelewe jambo hili:

*"Eliya alikuwa* ***mwanadamu mwenye tabia moja na sisi****, akaomba kwa bidi mvua isinyeshe, na mvua haikunyesha juu ya nchi muda wa miaka mitatu na miezi sita."* Yakobo 5:17

Eliya huyu aliyeshusha moto kwenye nyakati na matukio tofauti; Eliya huyu mwenye ishara na maajabu yasiyo ya kawaida… alikuwa mwanadamu kama wewe! Ni rahisi sana kumsoma Eliya kwenye maandishi kuliko ungeishi naye. Ungeona ubinadamu wake mwingi kiasi cha

kujaribia kuachana naye kwa kuwa *"mbona yeye na mimi hatuna tofauti"*. Hiyo sentensi ndiyo machinjio ya hatima za wafuasi wengi sana. Hauwafuati watu wasio watu bali unawafuata watu, kama wewe!

Utaona madhaifu yake, mambo anayohangaika nayo, mambo ambayo hajayaweza bado… pia utaona tabia za kawaida za wanadamu wote – kuchoka, kulala, kusikia njaa… utamsikia anacheka kicheko cha kibinadamu, kuna nyakati analia, anapiga miayo, na unaweza kumuona anaenda msalani. Je, utafifisha au kuondoa heshima uliyonayo kwake?

Usipokuwa mvumilivu katika kufuata, unaweza ukaikataa na kuitupa mbali neema kwa kukwaza na ubinadamu wa unayemfuata.

Kwa kuwa si lengo sana la kitabu hiki kuendea mada hii kwa kina, nikushauri usome machapisho ya mwandishi Roberst Liardon kuhusu God's Generals, akielezea mahali pao pa ufaulu na mahala walipoangukia. Itakumulikia mwanga zaidi kwenye jambo hili.

Huwa ninawafunza wafuasi ya kwamba, kumsogelea kwa karibu mtu wa Mungu kwa hasara yako iwapo haujui namna ya kuubeba ukaribu huo.

# SURA TA TANO:

# Thawabu ya Kufuata Mtu

1. Mtiririko wa uendelevu baraka

*“Wala haikanushiki kabisa kwamba mdogo hubarikiwa na mkubwa.”* Waebrania 7:7

Ufalme wa Mungu unatenda kazi kwa mtiririko na mpangilio. Si sehemu ya hovyo hovyo. Mukatdha wa andiko linalorejelewa hapo juu, ni baada ya Ibarahimu kushinda vita hatimaye alipaswa kutoa sehem ya kumi ya nyara alizoteka. Ilitakiwa, kimpagilio, atoe sehemu hiyo kwa mtu amabye ni mkubwa kuliko yeye. Ndiyo maana Mungu akatokeza mtu wa ghafla – mfalme wa Salemu, Melkizedeki. Ili apokee na kumbariki Ibrahimu.

Kwa minajiri hiyo basi, kanuni ya mkubwa kumbariki mdogo ikatimilizwa.

Kwenye mambo ya mwilini, jambo hili hueleweka na watu wengi kila nifundishapo. Nimewahi kuuliza mahala pengi, ni lini umesikia mzazi (baba au mama) amenunua vazi, chakula, au zawadi yoyote kisha anaipeleka kwa mtoto wake ili mtoto huyo amtamkie mzazi baraka? Kwa lugha nyingine, waza hivi, moja wa wazazi wako akuijie akiwa na sadaka mikononi mwake, kisha afike na kupiga magoti kuikabidhi na kukuomba umnenee baraka… Je,

utakubali? Je, utaweza kutamka baraka? Je, Baraka utakazomnenea zitatukia halisi? La hasha!

Hii ni kanuni ya kiroho iliyonakiliwa katika maswala ya mwilini. Utartibu ni kwamba mdogo hubarikiwa na mkubwa… **wala haikanushiki kabisa!** Tuna jambo tena la kujadiliana hapo? Jadili kwa hasara yako mwenyewe.

Umeshawahi kusikia sentensi ya watu kuuliza, "Hivi huyu mtoto ana wakubwa kwao?"

Nami ninakuuliza, hivi una wakubwa kwenu? Una mamlaka za kukunenea baraka? Au kwenu ninyi nyote ni wakubwa; wote ni sawa tu.

Kwa kila anayefuata, mtiririko wa Baraka utamfuata!

2. Uambukizo wa roho ya hekima

Mojawapo ya thawabu ambayo humwendea mtu anayefuata mtu ni uambukizo wa roho ya hekima. Kuna tofauti kati ya hekima na roho ya hekima. Cha kwanza ni mtoto na cha pili ni mzazi. Roho ya hekima ndiyo huzaa hekima kwenye maisha ya mtu kila mara itakapohitaji. Hata kwenye maeneo ambayo kiuhalisia unafahamika ya kwamba huna hekima; ukiwa na roho ya hekima utashangaa kuona imezaliwa hekima kwenye eneo hilo.

*"Na Yoshua, mwana wa Nuni, alikuwa amejaa roho ya hekima; maana Musa alikuwa amemwekea mikono yake juu yake; wana wa Israeli wakamsikiliza, wakafanya*

*kama BWANA alivyomwamuru Musa."* Kumbukumbu la Torati 34:9

Si ajabu Yoshua alipata matokeo aliyoyapata. Wana wa Israeli walimsikiliza. Hii ni zaidi ya kusikia sauti yake bali ni kuelewa ujumbe wake na kuingia kwenye hatua za utekelezaji.

Sasa fikiria hauna Musa wa kumfuata muda wote na kukuonyesha (expose) kwenye utendaji wa kiungu na kukuwekea mikono? Utatumia muda mwingi sana na jasho jingi sana kujieleza bele ya wana wa Israeli. Ni vizuri uelewe ya kwamba hawa wana wa Israeli wanaotajwa hapa ni zaidi ya watu milioni tatu kwa makadirio. Kusikilizwa na kundi kubwa namna hii la watu si jambo dogo.

3. Kupokea karama

Moja ya jambo linalonishangaza sana kuhusiana na mojawapo wa mababa wa kiroho kwenye maandiko matakatifu, Mtume Paulo, ni ujasiri wa kuyataja mambo kwa uwazi na kama yalivyo. Hebu tazama maandiko haya.

*"Usiache kutumia karama ile iliyomo ndani yako, uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya wazee."* 1Timotheo 4:14

Neno *"...karama ile..."* linaonyesha uelewa wa pamoja kati ya Paulo na Timotheo. Kwamba wanakubaliana na

wanajua ni karama gani hasa wanayoiongelea. Sasa, Paulo anaitaja karama husika na kutaja namna ilivyopatikana. Ni kwa kuwekewa mikono na wazee. Ni kama kumtahadharisha Timotheo ya kwamba asidhani aliipokea kwa namna nyingine yoyote. Hebu fikiria kama hauna wazee wa kukuwekea mikono?

*"Kwa sababu hiyo nakukumbusha, uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu."* 2 Timotheo 1:6

Halafu sasa, hapa anachora mstari mwingine. Kuna karama ya Mungu ndani ya Timotheo na namna ilivyopatikana ni kwa kuwekewa mikono na baba yake, mtume Paulo.

Mpaka sasa, walau tumetambua karama mbili zilizokuwa zikitenda kazi ndani ya Timotheo. Hazitajwa utendaji wake ni upi hasa, bali tumeonyeshwa mfumo uliotumika kuziingiza ndani yake. Kwa kuwekewa mikono na wazee na kwa kuwekewa mikono na Paulo… Ndiyo, ni karama za Mungu! Zimewekwa ndani ya mtu kwa mikono ya watu.

Kuna watu wakikuwekea mikono unapata karama na akuna watu wakikuwekea mikono unapata upara!

Una mtu ambaye unamfuata ambaye aweza kukuwekea mikono ili kuambuza karama/utendaji wa kimungu kwenye maisha yako? Au wewe unamfuata Roho wa Mungu tu?

Tusogee hatua moja mbele juu ya jambo hili. Angalia tena anachokisema mtume Paulo kwa kanisa la Rumi.

*“Kwa maana ninatamani sana kuwaona, nipate kuwapa karama ya rohoni, ili mfanywe imara.”* Warumi 1:11

Kisha tazama kile analisemesha kanisa lililoko mji wa Korintho.

*“Nami nikiwa na tumaini hilo nalitamani kufika kwenu hapo kwanza, ili mpate karama ya pili.”* 2 Wakorintho 1:15

Umegundua ya kwamba, hapa hajasema kuhusu kuwawekea mikono? Bali anaonyesha kwa uwepo wake kwenye maisha yao. Kwa kukaa naye na kumsikia na kumwona tu, kuna uambukizo wa karama ya rohoni hutokea.

Si mara zote baba yangu, askofu Goodluck Kyara, huniita kuniwekea mikono. Kuna nyakati ambazo nikiwa naye ana kwa ana, au nikimsikiliza akifundisha kanisani; hata nikiongea naye kwa simu tu; nikisikiliza mfundisho yake; nikisoma mafundisho aliyoandika… huwa ninasikia uambukizo wa utendaji wa kiungu kwenye maisha yangu.

Aina hii ya watu haukutani nao kama *“marafiki”* zako wa siku zote, la sivyo utapishana na uambukizo wa mambo ya rohoni. Huwa ninakutana nao huku ndani yangu nikiwa nimepania sana kupokea jambo la kiungu.

4. Kubadilishwa jina na hadhi

*"Na Yusufu, aliyeitwa na mitume Barnaba, (maana yake, mwana wa faraja), Mlawi, asili yake ni mtu wa Kipro."* Matendo ya Mitume 4:36

Huyu ndugu alipewa jina na wazazi wake, Yusufu. Mitume waliona hatima ndani yake. Walimwona kama mwana wa faraja, wakampa jina. Muda si mrefu akaanza kutenda sawa na jina lake jipya. Kutokea kwenye maandiko, tunaona namna gani alimchukua Paulo baada ya kuokoka na kutokukubaliwa kwa urahisi na jamii ya waaminio kwa sababu ya historia yake ya kuliudhi na kulisababishia dhiki kanisa la Kristo.

*"37. Barnaba akaazimu kumchukua Yohana aliyeitwa Marko pamoja nao. 38. Bali Paulo hakuona vema kumchukua huyo aliyewaacha huko Pamfilia, asiende nao kazini. 39. Basi palitokea mashindano baina yao hata wakatengana. Barnaba akamchukua Marko akatweka kwenda Kipro."* Matendo ya Mitume 15:37-39

Nimetamani uone anachokitenda Barnaba. Alianza kwa Paulo na sasa anakitenda kwa Yohana Marko. Wale ambao kwa namna moja au nyingine hawakubaliki au kupokelewa kwa urahisi, yeye huwa upande wao. Huwafinyanga kiasi cha kufaa na kukubalika kwa ajili ya utendaji wa huduma.

*"Luka peke yake yupo hapa pamoja name. Umtwae Marko, umlete pamoja nawe, maana anifaa kwa utumishi."* 2 Timotheo 4:11

Tazama Marko yuleyule aliyeonekana hafai kwa utumishi, sasa anafaa. Tena anafaa kwa mtu yuleyule aliyemkataa awali, Paulo. Ni kwa sababu tu amekaa kwenye mikono ya mwana wa faraja, Barnaba.

Umegundua ya kwamba mitume hawakumpa jina tu kama almaarufu (a.k.a)? Walimpa jina lililogeuza hali na hadhi yake jumla.

Tazama mtu mwingine aitwaye Epafrodito.

*"25. Lakini naliona imenilazimu kumtuma kwenu Epafrodito, ndugu yangu, mtenda kazi pamoja name, askari pamoja name; tena ni mtume wenu na mhudumu wa mahitaji yangu. 29. Mpokeeni, basi, katika Bwana, kwa furaha yote, mkawahesabu watu kama huyu kuwa watu wa kuheshimiwa…."* Wafilipi 2:25-30

Chanzo cha heshima ya Epafrodito ni ufuasi wake wa kina kwa mtume Paulo. Ukitaka kuelewa kwa mapana kuhusu mtu huyu wa thamani sana wa Bwana Yesu, hakikisha unasoma kitabu cha Mfuasi Mfano wa Epafrodito.

*"Mungu aliweka wito ndani yangu wa kwenda kumtumikia mtu wa Mungu, askofu Oyedepo; mtu wa Mungu akaniita kuwa mchungaji."* Askofu David Abioye

Nani asiyejua mgeuko na nafasi kubwa ya kiuongozi kwenye ukristo wa Afrika aliyonayo Askofu Abioye? Ni matokeo ya ufuasi wake kwa mtu wa Mungu, askofu Oyedepo.

# SURA YA SITA:

## Ufuasi katika Utekelezaji

1. Bainisha watu unaowafuata – kwenye ngazi husika (baba, waalimu, vielelezo)
2. Pima kiwango chako cha ufuasi
3. Weka azimio la kupandisha kiwango chako cha ufuasi
4. Weka azimio la kuwafuata unaotakiwa kuwafuata kwa bidii

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Youtube: James Kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

NEW VINE CHURCH Dodoma

# Abudu Nasi

**KILA JUMAPILI - saa 3.00 asbh -6.30 mch**

**KILA ALHAMISI - saa 11.00 jioni -12:15 jioni**



nvc_dodoma    +255 754 917 764

Mahali tulipo: **Swaswa - Njia Panda ya Waziri Mkuu**

*A Home of Impact*

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake; ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; Baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764